

MKATABA WA KUPANGISHA NYUMBA

MKATABA HUU wa kupangisha nyumba umefanyika leo tarehe 01 Mwezi wa 06, mwaka 2024.

BAINA YA

NAOMI WILLIAM MATINDE wa Dar es salaam (ambaye kwa madhumuni ya mkataba huu ataitwa {"**MWENYE NYUMBA**"}) kwa upande mmoja,

EASTERN MINING LIMITED wa Dar es salaam (ambaye kwa madhumuni ya mkataba huu ataitwa {"**MPANGAJI**"}) kwa upande mwingine.

KWA KUWA, MWENYE NYUMBA ni mmiliki halali wa nyumba iliyopo kwenye mtaa wa Bonde la Mpunga iliyopo eneo la, **Msasani, Dar es Salaam**

NA

KWA KUWA mwenye nyumba kwa hiari yake mwenyewe ana nia na madhumuni ya kupangisha nyumba iyo kwa mpangaji na mpangaji kwa hiari yake mwenyewe anakubali kupangishwa kwenye nyumba hiyo,

HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA MAKUBALIANO YAFUATAYO: -

1. Kwamba, kodi ya pango ya shilingi Laki SABA tu (700,000/=) kwa mwezi, mwenye nyumba anampangisha mpangaji na mpangaji anapanga nyumba hiyo kwa ajili ya makazi.
2. Kwamba, Mkataba huu ni wa miezi sita na utanza Tarehe 01/06/2024 na utaisha 31/06/2025
3. Kwamba, mpangaji atatakiwa kulipa kodi yote ya miezi sita.
4. Kwamba, malipo yote kwa ajili ya nyumba hiyo tajwa yamelipwa na mpangaji kama makubaliano yao na wamekubaliana kusainisha mkataba huu.

MPANGAJI ANAAHIDI nakuthibitisha kama ifuatavyo: -

5. Kwamba, atalipia gharama zote za umeme, maji, maji taka, takataka, ulinzi pamoja na nyinginezo zinazohusiana na mazingira bora ya nyumba, katika mamlaka husika na kwa kipindi chote atakachodumu kwenye Mkataba huu.
6. Kwamba, makubaliano ya mpangaji na mwenye nyumba ni kwamba mwenye nyumba atapaka rangi ndani na nje ya ukuta (fence) kwa mwezi wa kwanza.
7. Kwamba, mpangaji atatumia nyumba hii aliyopanga kwa dhumuni lililoko kwenye makubaliano ya kuishi na sio vinginevyo kwa jinsi na namna ambavyo pande zote mbili zimeridhiana katika mkataba huu.
8. Kwamba, atatumia nyumba hiyo na kuiweka katika hali ya usafi wakati wote, na vile vile atayaweka mazingira ya nyumba yake katika hali nzuri na pia haruhusiwi kufanya marekebisho yoyote yale makubwa bila idhini ya maandishi ya mwenye nyumba.

9. Kwamba, hatompangisha mtu mwingine nyumba hiyo aliyopangishwa bila idhini ya maandishi toka kwa Mwenye Nyumba.
10. Kwamba, mpangaji anaahidi kulipa kodi kwa wakati na kwa kadri ya makubaliano yake na mwenye nyumba.
11. Kwamba, atalipia fidia uharibifu wowote utakaotokana na uzembe wa Mpangaji au wahusika wake.

MWENYE NYUMBA anaahidi na kuthibitisha kama ifuatavyo: -

12. Kwamba, hatomsumbua wala kumbugudhi Mpangaji katika nyumba hiyo kwa kipindi chote ambacho mpangaji atakuwa anaishi katika nyumba hiyo baada ya kuwa amelipa kodi.
13. Kwamba, atahusika kulipia kodi ya Kiwanja, kodi ya majengo pamoja na kodi nyingine zinazomhusu.

MWENYE NYUMBA na **MPANGAJI** kwa pamoja wanakubaliana kwamba: -

14. Mkataba, huu wa upangishaji ni wa muda maalum wa miezi sita tu, ambao unaweza kuongezwa kwa makubaliano ya pande zote mbili.
15. Kwamba, mkataba huu utahesabika kuwa umevunjika kabla ya wakati ikiwa upande wowote katika mkataba huu utavunja masharti yalioanishwa kwenye vipengele vya mkataba huu.

USULUHISHI WA MIGOGORO

16. Kwamba, wakati wowote endapo kutatokea kutoelewana kwa namna yoyote kati ya mwenye nyumba na Mpangaji basi wahusika wanapaswa kukaa pamoja na kutafuta suluhisho kwa njia ya majadiliano na kwamba endapo upande wowote ule kwa sababu zake zenyewe utagoma kukaa na upande mwingine kupata suluhu, basi Mkataba huo utakuwa umefikia tamati na kwamba upande utakaokuwa umesababisha kuvunjika kwa Mkataba huu utabeba madhara ya uvunjifu wa Mkataba huu.

MAJANGA YA ASILI

17. Masharti ya mkataba huu yatakaposhindwa kutekelezwa kutokana na majanga ya asili, basi hakuna upande wowote katika mkataba huu utakaohesabika kuhusika katika kuvunja mkataba huu.
18. Endapo kutatokea majanga ya asili, pande zote mbili zitakaa kwa pamoja na kujadili namna njema ya kuendelea na Mkataba huu kwa dhamira ya kutekeleza masharti na matakwa ya

Mkataba huu. (*Majanga ya asili kwa mujibu wa mkataba huu ni kama vile moto usio wa uzembe, mafuriko, njaa nk.*)

SHERIA

19. Mkataba huu unasimamiwa na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

KWA USHUHUDA wa yaliyoelezwa hapo juu, pande zote mbili wanatia saina makubaliano haya kuthibitisha kuwa wamesoma, kuelewa na kukubaliana na masharti yaliyomo katika mkataba huu:

Umesainiwa Dar es Salaam na
NAOMI WILLIAM MATINDE

ambaye namfahamu binafsi

leo tareheMwezimwaka 2024.

.....
MWENYE NYUMBA

MBELE YANGU

Jina: RAHIMU MWAYA BAKARI

Anwani: DAR ES SALAAM

Cheo: WAKILI



Umesainiwa hapa Dar es Salaam na **BAILI SUN**

For EASTERN MINING LIMITED ambaye
namfahamu binafsi
ambaye namfahamu binafsi leo
tarehe 01.....Mwezi06.....mwaka, 2024.

.....
MPANGAJI

MBELE YANGU

Jina: RAHIMU MWAYA BAKARI

Anwani: DAR ES SALAAM

Cheo: WAKILI



Rahimu Mwaya Bakari